

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



SIMU NA MAKUNDI YA WHATSAPP YATUMIKA KUFANYA UDANGANYIFU KATIKA MITIHANI YA VETA KAGERA

TAARIFA KWA UMMA

DESEMBA 15, 2020

1.0 Utangulizi

Ndugu wanahabari,

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kagera tumeendelea kutekeleza majukumu yetu kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya mwaka 2007. Katika utekelezaji wa majukumu yetu tumeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa mapambano dhidi ya Rushwa wakiwemo waandishi wa habari, viongozi wa Serikali na wananchi kwa ujumla. Aidha majukumu haya yametokelezwa katika wilaya zote zilizo ndani ya Mkoa wa Kagera.

Ndugu waandishi wa habari,

Tunapenda kuujulisha umma kuwa tunawashikilia wanafunzi **38** wa Chuo cha Ufundi VETA kilichpo katika Manispaa ya Bukoba pamoja na wakufunzi wao wawili ambao walikuwa wasimamizi wa mitihani (ambao ni **Francis Mwangosi na Ssenabulya Daud**) pamoja na Mkuu wa Chuo hicho cha Ufundi - VETA aitwaye **Baluhi Mayala Mitinje** kwa makosa ya kufanya udanganyifu katika mitihani na matumizi mabaya ya ofisi kinyume na kifungu cha 31 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007 pamoja na makosa ya

kuvujisha mtihani chini ya Vifungu vya 18, 20 na 23 vya Sheria ya Baraza la Mitihani la Taifa, Sura 107 R:E. 2019

Aidha sanjari na kuwashikilia wanafunzi na wakufunzi hao ambao tumewakamata wiki iliyopita katika operesheni maalum tuliyoifanya, pia tumekamata jumla ya **simu 41 amabapo 38** ni za wanafunzi na simu 3 za wakufunzi ambazo wanafunzi hao walikuwa wameingia nazo katika chumba cha Mtihani wa Taifa wa Elimu ya Ufundi. Simu hizi zilikuwa zinatumiwa na wanafunzi waliokuwa katika chumba cha mitihani - kurusha maswali kwa wakufunzi ambao walikuwa ofisini kwao ambapo walijibu maswali hayo na kisha kuwatumia wanafunzi majibu husika wakiwa katika Chumba cha Mtihani.

Ndugu wanahabari,

Pamoja na kuwashikilia wanafunzi hao 38 wa Chuo cha VETA Kagera pia TAKUKURU mkoa wa Kagera tunawashikilia wanafunzi wengine 21 wa Chuo cha Tuinuane VTC pamoja na wakufunzi wao wawili ambao ni **Mwl Charles Byabachwezi** na **Verdiana Myaka** pamoja na Mkuu wa Chuo hicho aitwaye **Emmanuel Jonas** kilichopo katika Kijiji cha Kabale Kata ya Karabagaine pamoja na wasimamizi wawili wa Mitihani ambao ni waajiriwa wa Chuo cha Ufundi - VETA Kagera.

Aidha wanafunzi wa chuo hiki cha Tuinuane pia wanatuhumiwa kwa makosa ya kuingia na simu katika Chumba cha Mtihani na kisha kutumia simu hizo kupiga picha maswali na kuyarusha kwa wakufunzi waliokuwa nje ya chumba cha mtihani ili kuwapatia majibu ya maswali hayo kwa njia ya makundi ya WhatsApp (Kabale VTC na Secret Magic) na ujumbe mfupi wa maneno. Makundi haya ya WhatsApp yalitengenezwa na wakufunzi na ndio wasimamizi wa makundi hayo(Admn)

Ndugu wanahabari

Katika chuo cha Tuinuane ambacho pia ni chuo kilichosajiliwa na VETA licha ya kukamata wanafunzi 21 pia tumeweza kukamata simu 21 za wanafunzi na simu 4 za wakufunzi pamoja na fedha taslimu 151,000/= fedha ambazo zilikuwa zimechangwa na wanafunzi kwa ajili ya kuwapatia wasimamizi wa mitihani hiyo ya taifa ya Elimu ya Ufundi.

Ndugu wanahabari,

Wanafunzi na wakufunzi tajwa wanashikiliwa kufuatia taarifa za kiintelijensia zilizobainishwa na TAKUKURU mkoa wa Kagera kuwa kumekuwepo na udandanyifu katika mitihani ya Taifa ya Elimu ya Ufundi katika Chuo cha Tuinuane VTC na VETA mkoani Kagera ambapo wakufunzi wamekuwa wakiwapatia majibu wanafunzi wanaokuwa katika vyumba vya mitihani kupitia simu zao za Mkononi na kwamba wanafunzi wamekuwa wakiruhusiwa kuingia na Simu za mkononi katika vyumba vya mtihani makosa ambayo ni kinyume cha Sheria.

Ndugu wanahabari,

Uchunguzi unaoendelea umebaini kuwepo kwa ukiukwaji mkubwa wa taratibu za Mtihani katika Chuo cha Ufundi VETA mkoani Kagera pamoja na Chuo cha Tuinuane VTC kunakofanywa na Wakuu wa Vyuo hivyo kwa kushirikiana na baadhi ya wakufunzi, wanafunzi pamoja na wasimamizi wa Mitihani - lengo likiwa ni kuwasadia wanafunzi wao na kutaka kuonyesha kuwa vyuo hivyo vinafanya vizuri.

Ndugu wanahabari,

WITO:

Tunatoa wito kwa wananchi wote wa mkoa wa Kagera kuendelea kushirikiana na TAKUKURU na Serikali kwa ujumla katika mapambano dhidhi ya Rushwa kwani Rushwa husababisha kupatikana kwa wataalimu wabovu na wasiofaa, huathiri uwajibikaji na uwazi katika utendaji, huathiri ufanisi na ubora wa elimu na husababisha uvunjifu wa haki za binadamu. Humong'onyoa imani ya Wananchi kwa Serikali yao na hudhoofisha maendeleo.

Ikumbukwe kuwa tunaweza kuwa na maendeleo endelevu iwapo **HAKI** itatawala miongoni mwetu kwa kuwa **HAKI** inainua Taifa lenye watu wenye **AMANI** na **FURAHA**. Pia tumebainisha kuwa **RUSHWA** inaondoa **HAKI**, na **HAKI** ikiondoka **AMANI** na **FURAHA** vitapotea. **AMANI** na **FURAHA** vikipotea hakuna **MAENDELEO** yoyote yatakayopatikana kwa Taifa na kwa mtu binafsi.

Signed
JOHN K.E JOSEPH
MKUU WA TAKUKURU (M)

